

FOCUS A365

Another Manyamfranchise.Com Evaluation Test

FORM 4 TERM 1 KISAHILI PP3 EXAMINATIONS 2018

NAME: _____ ADM NO: _____ CLASS: _____

MAAGIZO

- a) Jibu maswali manne pekee
- b) swali la kwanza ni la lazima
- c) maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki
- d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
- e) Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
- f) Kila swali lina alama Ishirini

SEHEMU A - LAZIMA

1. FASIHI SIMULIZI

- a) Fanani huwa na nafasi mbili katika usimulizi wa hadithi
Taja na ueleze kila nafasi (al 4)
- b) Fafanua aina zifuatazo za ngano(al 4)
 - i) Istiara
 - ii) Mbazi
- c) Methali na vitendawili hufanana kwa kiwango Fulani. Toa mifano sita inayodhihirisha kauli hii(al 12)

SEHEMU B – RIWAYA

KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA

(Jibu swali la 2 au la 3)

2. Wahusika wengi riwayani walilala wakaamka wakiwa wamebadilika. Thibitisha (al 20
AU
3. “Dunia imepasuka ufa mkubwa usiozibika alaa kulihali.”
 - i) Weka dondoo hili katika muktadha wake(al 4)
 - ii) Eleza mbinu mbili za lugha zilizotumika (al 4)
 - iii) Thibitisha ukweli kuwa dunia imepasuka ufa mkubwa usiozibika kwa kumulika matukio Riwayani.
(al 12)

SEHEMU C – TAMTHILIA

KIGOGO – Pauline Kea

(Jibu swali la 4 au la 5)

4. Masaibu ya wanasagamoyo ni taswira ya masaibu wanayopitia wanajamii katika Bara la Afrika. Jadili (al 20
5. “Si wajua hesabu nzuri ni ya kutia na kutoa”
 - a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al 4)
 - b) Tambua tamathali ya usemi inayojitokeza katika dondoo hili (al 2)
 - c) Kwa kurejea tamthilia ya kigogo, fafanua mambo saba yanayopiganiwa na wanasagamoyo
(al 14)

SEHEMU D – USHAIRI

Jibu swali la 6 au la 7

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo

LONGA

Longa longea afwaji, watabusarika
Longa uwape noleji, watanusurika
Longa nenea mabubu, Sema na viduko

Longa usichachawizwe, tamka maneno
Longa usitatanizwe, mbwa aso meno
Longa usidakihizwe, kishindo cha funo

Longa yote si uasi, si tenge si noma
Longa pasi wasiwasi, ongea kalima
Longa ukuli kwa kasi, likate mtima

Longa zungumza basi, liume ja uma

Longa japo ni kombora, kwa waheshimiwa
Longa liume wakora, kwani wezi miwa

Longa bangu na papara, hawakuitiwa
Longa bunge si kiwara, si medani tawa
Longa simba marara, wanaturaruwa.

Maswali

- a) Tambua na ueleze nafsi neni katika shairi hili (al 1)
- b) Onyesha vile kibali cha utunzi wa mashairi kilivyotumika kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (al 4)
- c) Kwa kutoa maelezo mwafaka, tambua bahari nne zilizotumika na mtunzi kwenye shairi hili. (al 4)
- d) Eleza aina tatu za urudaji katika shairi (al 3)
- e) Tambua na kueleza toni ya shairi (al 2)
- f) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi (al 2)
 - i) Afwaji
 - ii) Tenge
- g) Eleza umbo la shairi hili (al 4)

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Nitafukuzwa mbinguni
Kwa ushairi wangu mbaya
Lakini hata motoni nitaimba:
Wanasema
Wanasiasa ni kama jizi
Lililosukuma mtoto pembeni
Na kunyonya ziwa la mama
Wakati amelala usingizi usiku.

Wasema
Mwanasiasa afapo
Tumejikomboa na domo
Moja pana lizibwalo na mchanga
Na kilima cha simenti ngumu
Lisikike tena hadharani.

Wanasema pia
Kusema haki
Kwa kawaida
Wanasiasa hatuwapendi.
Kupiga kura ni hasira za mkizi
Ni basi tu. Ni Ah!
Ah!
Wanamalizia
Nchi mmefilisi waacheni walimu
Wakajenga taifa jipya

Kama hamwezi kuona mbali

Bure kuweka mkono usoni,
Bure hakuna kichwa
Kama hamwezi kufikiri.

Ng'ombe amekamuliwa na wazungu
Waarabu, wahindi na wao
Sasa anatoa damu
Vilivyobaki ni chai ya rangi
Na mdomo mapana zaidi
Yaliyo bado hai.
Kuimba nimeimba.

Maswali

- a) Mshairi ana dhamira gani?(al 2
- b) Shairi hili ni la kukatisha tamaa, tetea rai hii (al 2
- c) Onyesha matumizi mawili ya mishata (al 2
- d) Eleza mbinu zozote nne za lugha zilizotumika katika shairi hili (al 4
- e) Andika ubeti wa mwisho katika lugha tutumbi. (al 4
- f) Fafanua umbo la shairi hili (al 3
- g) Eleza maana ya mafungu ya maneno yafuatayo: (al 3
 - i) Kupiga kura ni hasira ya mkizi
 - ii) Kuweka mkono usoni
 - iii) Ng'ombe amekamuliwa.